TANGAZO LA SERIKALI Na.508 la Tarehe 14/9/2018

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa Chini ya Kifungu Cha 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO ZA (USHURU WA MINADA YA MIFUGO) ZA HALMASHAURI YA MJI KONDOA, 2018

Jina na Mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Minada ya Mifugo) za Halmashauri ya Mji Kondoa za Mwaka 2018, na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelekezwa vinginevyo;-

"*Afisa Mwidhiniwa* maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"*Halmashauri*" maana yake ni Halmashauri

ya Mji Kondoa.

*"Mifugo"* maana yake ni ng'ombe, mbuzi, kondoo, punda pamoja na aina nyingine yoyote ya wanyama wengine wafugwao na binadamu.

*"Mkurugenzi"* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

Kuanzisha Minada

4. (1) Halmashauri itaanzisha na kutangaza maeneo maalum yatakayotumika kama minada ya mifugo kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila ya kuathiri Masharti ya kifungu cha 4 (1) cha kifungu cha 4 Halmashauri inaweza kufuta maeneo ya shughuli za minada ya mifugo kwa kadri itakavyoona inafaa.

Ushuru wa Mifugo

5. (1) Halmashauri itatoza Ushuru wa Mifugo mnadani kama ilivyoelekezwa katika jedwali la pili la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ushuru utakaotozwa chini Sheria Ndogo hizi utalipwa baada ya mifugo kuuzwa na utalipwa na mnunuzi

Muda wa kufungua Minada

6. (1) Muda wa kukusanya Ushuru na kuanza shughuli za mnada utakua ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi (12:00) na kumalizika saa kumi na mbili jioni (12:00).

(2) Halmashauri itatenga siku maalum za kila mnada kwa kuzingatia jiografia ya maeneo ya minada kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la tatu la Sheria Ndogo hizi

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu 6(1) cha Sheria Ndogo hizi, Afisa Muidhiniwa au Wakala anaweza kukusanya ushuru kabla au baada ya muda uliotajwa endapo atakua na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi.

(4) Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(5) Uuzaji na ununuzi wa mifugo yote katika maeneo ya Halmashauri utafanyika katika minada iliyoanzishwa chini ya Sheria Ndoho hizi.

Mabadiliko ya viwango vya Ushuru

7. (1) Endapo itaonekana kuwa inafaa, Halmashauri itaweza kubadilisha viwango vya ushuru kwa kufuta, kurekebisha au kuweka viwango vipya.

(2) Katika kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa minada au kipengele chochote katika Sheria Ndogo hizi, Halmashauri itafuata taratibu zote za utungaji wa Sheria Ndogo zinazoelekezwa na Sheria ya Serikali ya Mitaa( Mamlaka za Miji) Sura ya 288.

Ukusanywaji wa Takwimu

**8.** Afisa Mwidhiniwa ataandaa na kuwasilisha kwa Halmashauri taarifa maalum itakayoonyesha idadi, aina na bei ya kila mfugo uliouzwa mnadani kwa madhumuni ya kutunza na kufanyia kazi takwimu hizo.

Katazo

**9.** Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kukataa aina yoyote ya mifugo au bidhaa kuingia na kuuzwa ndani ya eneo la mnada iwapo mifugo hiyo au bidhaa hizo zinaweza kuhatarisha afya, au usalama wa mifugo mengine au watumiaji wa eneo la Mnada.

Magari yanayoingia mnadani

**10.** Halmashauri itatenga maeneo maalumu ya kushusha na kupakia mizigo na eneo la maegesho ya magari yatakayoingia mnadani.

Kusafirisha Mifugo

**11.** Halmashauri itatoza ada ya kibali maalum cha kuruhusu kusafirisha mifugo ndani au nje ya eneo la Halmashauri ambacho kitaonesha Idadi ya mifugo inayosafirishwa, njia au utaratibu utakaotumika kusafirisha mifugo hiyo.

Uthibiti wa biashara ya Mifugo

**12.** (1) Halmashauri itadhibiti biashara ya kuuza na kununua mifugo kwa kuweka taratibu zifuatazo;-

(a) mifugo yote itauzwa katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya minada;

(b) kutoza ushuru wa mifugo itayouzwa minadani;

(c) kutoa na kukagua vibali vyote vya kusafirisha mifugo; na

(2) Wafanyabiashara ambao watakua na vibali vilivyotolewa na mamlaka nyingine, kabla ya kuanza biashara ya kuuza na kununua mifugo watatakiwa kuwasilisha vibali vyao kwa Halmashauri kwa ajili ya uhakiki;

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 6(2) cha Sheria Ndogo hizi, wafanyabiashara hao watalazimika kutekeleza masharti yaliyowekwa kwenye Sheria ndogo hizi.

(4) Mifugo itakayoonekana kusafirishwa nje bila kupata kibali itakamatwa na kurejeshwa nchini na hatua nyingine za kisheria zitafuatwa ikiwemo kufungua shauri mahakamani.

Wajibu kwa Halmashauri wa kulipa fidia

13. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kulipa fidia ya hasara itakayosababishwa na Afisa Mwidhiniwa itakayotokana na uzembe wa makusudi wakati wa kukusanya Ushuru au wakati wa kutekeleza Sheria Ndogo hizi.

Kufifilisha Makosa

14. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyochopungua shilingi laki mbili (Tsh.200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (Tshs. 500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa faini anayodaiwa kama itakavyoelekezwa kwenye jedwali la pili la Sheria Ndogo.

Adhabu

15. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/= na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) jela na kisichozidi miaka miwili (2) jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 4(1)*

ORODHA YA MINADA

| Na. | Jina La Mnada | Mtaa / Kijiji | Kata |
|---|---|---|---|
| 1. | BICHA | BICHA | KILIMANI |
| 2. | KOLO | KOLO | KOLO |
| 3. | IYOLI | IYOLI | KINGALE |

JEDWALI LA PILI

USHURU WA MIFUGO

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 5(1)*

| Na. | Aina ya Mifugo | Kiasi cha Ushuru Utakaotozwa |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | Tsh 2000/= |
| 2. | Mbuzi | Tsh 1500/= |
| 3. | Kondoo | Tsh 1500/= |
| 4. | Nguruwe | Tsh 2000/= |
| 5. | Kuku , bata, sungura | Tsh 500/= |
| 6. | Bidhaa ambazo si mifugo | Tsh 1,000/= |
| 7. | Mifugo mingine ambayo haikutajwa | Tsh. 500 |

JEDWALI LA TATU

MUDA NA SIKU ZA MINADA

*(Limetungwa Chini ya kifungu cha 6(2)*

| Na. | Jina la Mnada | Siku ya Mnada | Muda wa kufunguliwa | Muda wa kufungwa |
|---|---|---|---|---|
| 1. | BICHA | Tarehe 4 na Tarehe 16 ya kila mwezi, na pia na Gulio kila Jumamosi | 12:00 Asubuhi | 12:00 Jioni |
| 2. | KOLO | Tarehe 2 kila mwezi | 12:00 Asubuhi | 12:00 Jioni |
| 3. | IYOLI | Tarehe 28 kila mwezi | 12:00 Asubuhi | 12:00 Jioni |

JEDWALI LA NNE

(Limetungwa Chini ya Kifungu cha 14)

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

mimi ............................................................................................... nakiri kwa hiari yangu mwenyewe mbele ya................................... ambaye ni mkurugenzi wa halmashauri ya mji kondoa kwamba mnamo tarehe ......... ya mwezi................. mwaka ............ nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha ................cha sheria ndogo za (ushuru wa minada ya mifugo) za halmashauri ya mji kondoa za mwaka 2018

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe .....................ya Mwezi ...........Mwaka .......

Jina: ..........................................................................................

Saini: ..............................................

Mbele ya: ....................................

Cheo: .............................................

Saini: ............................................

Tarehe: .........................................

Nembo ya Halmashauri ya Mji wa kondoa imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe 13/5/2017 mbele ya:-

KHALIFA KONDO
*Mkurugenzi wa Mji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

L.S

HAMZA MAFITA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa*

NAKUBALI,

DODOMA,
15 Agosti, 2018

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*